MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 14/07/2022 KATIKA UKUMBI MKUBWA WA MANISPAA

KU/SMC/BM/80/2022 – WALIOHUDHURIA:

A. WAHESHIMIWA MADIWANI

1.	Mhe. Jastin Malisawa	-	Mstahiki Meya – Mwenyekiti
2.	Mhe. Istus Kapufi	-	Naibu Meya
3.	Mhe. Dimela Kafwa	-	Diwani viti Maalum
4.	Mhe. Juma Mnanka	-	Diwani Kata ya Msua
5.	Mhe. Adorfina Konongo	-	Diwani Kata ya Lwiche
6.	Mhe. Frank Lupimo	-	Diwani Kata ya Milanzi
7.	Mhe. Francis Manyika	-	Diwani Kata ya Majengo
8.	Mhe. Mary Kipalasha	-	Diwani Kata ya Malangali
9.	Mhe. Hadija Maufi	-	Diwani Viti Maalum
10.	Mhe. Edwin Misasi	-	Diwani Kata ya Katandala
11.	Mhe. Roswita Chekwe	-	Diwani Viti Maalum
12.	Mhe. Janeth Sinyangwe	-	Diwani Viti Maalum
13.	Mhe. Colnel Kafumu	-	Diwani Kata ya Sumbawanga
14.	Mhe. Anthony Kayombo	-	Diwani Kata ya Chanji
15.	Mhe. Gabriel Kimamala	-	Diwani Kata ya Izia
16.	Mhe. Charles Chakupewa	-	Diwani Kata Ya Momoka
17.	Mhe. Andrea Cheka	-	Diwani Kata ya Kizwite
18.	Mhe. Juma Dawood Nzegere	-	Diwani Kata Mazwi
19.	Mhe. Agustino Ngoani	-	Diwani Kata ya Ntendo
20.	Mhe. Syriacus Pangani	-	Diwani Kata ya Kasense
21.	Mhe. Cardius Mtullo	-	Diwani Kata ya Pito
22.	Mhe. Leticia Kipeta	-	Diwani Viti Maalum
23.	Mhe. Sangu Maarifa	-	Diwani Kata Mollo
24.	Mhe. Anna Mwamba	-	Diwani Viti Maalum
25.	Mhe. Lameck Pondamali	-	Diwani Kata ya Mafulala

B. WATAALAM

1.	Ndg. Jacob J. Mtalitinya	-	Mkurugenzi wa Manispaa Katibu
2.	Ndg. Frank Mateni	-	Afisa Maendeleo ya Jamii
3.	Ndg. Khadija Dalasia	-	Afisa Mawasiliano
4.	Ndg. Eliud Fungo	-	Kaimu Afisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi
5.	Ndg. Ndaro Samson	-	Mchumi Manispaa

6. Ndg. Adam Evarist - Afisa Michezo
7. Ndg. Samson Medda - Afisa Utumishi na Utawala
8. Ndg. Thadeo Maganga - Afisa Maliasili na Utalii
9. Ndg. George Nyanga - Afisa Usafirishaji
10. Ndg. Deogratius Masalu - Mkaguzi wa Ndani
11. Ndg. Derick Sikale - Kaimu Afisa Elimu Msingi
12. Ndg. Asha Milasi - Afisa Manunuzi
13. Ndg. Fortunatus C. Lyapa - TSC
14. Eng. John Myovela - Kaimu Mhandisi wa Ujenzi
15. Ndg. Jenifrida Manuma - Afisa TEHAMA
16. Ndg. Mathew Madama - Mwanasheria Manispaa
17. Dr. Witness Mbwelwa - Kaimu Mganga Mkuu
18. Ndg. Richard Mkandarasi - Afisa Biashara Manispaa
19. Ndg. Kerry Mwansele - Kaimu Mweka Hazina
20. Ndg. Mwajabu Abdulahiman - Kaimu Afisa Mazingira
21. Ndg. Hebel Kibona - Afisa Elimu Sekondari

C: WAALIKWA

1. Ndg. Sebastian Waryuba - Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga
2. Ndg. Neema Fungo - Jeshi la Akiba
3. Ndg. Sabina Mwajeka - Afisa Tarafa Itwelele
4. Ndg. Dafroza Msechu - Ag. DAS
5. Ndg. Emmanuel Gelson - UHAMIAJI
6. Ndg. Ismail Mwinyi - Afisa Usalama Wilaya
7. Ndg. Gabriel Zunda - Kaimu Mkuu wa Polisi Wilaya
8. Ndg. Joseph Mzumala - Magereza
9. Ndg. Tabu Shaaban - Katibu CCM Wilaya
10. Ndg. Chami Chasuka - Mwenyekiti CCM

11. Ndg. Festo Felician	-	Mwenyekiti CHADEMA
12. Ndg. Alfred Kapufi	-	Katibu CHADEMA
13. Ndg. Magreth Chipeta	-	Afisa Serikali za Mitaa
14. Ndg. James Mbungano	-	TAKUKURU
15. Ndg. Peti Siyame	-	ITV
16. Ndg. Sammy Kisika	-	AZAM TV
17. Ndg. Edith Peter	-	VOS
18. Ndg. Misri Mwasenga	-	STAR TV
19. Ndg. Peter Malema	-	Global TV
20. Ndg. Paul Mathias	-	Mwananchi
21. Ndg. Lusajo Mboli	-	Zimamoto
22. Major A.B Yobela	-	Mshauri wa Mgambo

D. SEKRETARIETI

1. Ndg. Maria Ntara	-	Katibu wa Vikao Manispaa
2. Ndg. Lilian Konjani	-	Katibu wa Vikao

KU/SMC/BM/81/2022 – KUFUNGUA KIKAO:

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afungue kikao, Mwenyekiti alianza kwa kusoma dua. Mwenyekiti alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kutufikisha siku ya leo ambapo alisema kuwa kikao cha leo ni kikao cha Kawaida cha robo ya nne 2022. aliomba wajumbe wazingatie kanuni katika kuchangia hoja katika kikao hiki. Mwenyekiti Alifungua kikao mnamo saa 7.00 Mchana.

KU/SMC/BM/82/2022 – KUTHIBITISHA DONDOO:
Ziliwasilishwa dondoo za kikao cha tarehe 14.07.2022 wajumbe kwa kauli moja walizipokea na kuzithibitisha.

KU/SMC/BM/83/2022 – MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MSTAHIKI MEYA NA MKURUGENZI

Hoja
Mhe. Leticia lipenda kufahamu katika Kata ya Mazwi mradi wa ujenzi wa barabara ya lami ni KM 0.3 na sio KM 15

Jibu
Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa KM 15 ni ujenzi wa barabara ya lami kwa Manispaa yote sio Kata ya Mazwi tu.

KU/SMC/BM/84/2022 – KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 01.06.2022

Muhtasari ulisomwa na kufanyiwa masahihisho ukurasa wa 3 na ukurasa wa 7 kisha Katibu na Mwenyekiti waliuwekea saini Muhtasari huo.

KU/SMC/BM/85/2022 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 01.06.2022

Iliwasilishwa taarifa ya maazio ya kikao cha tarehe 01.06.2022 na wajumbe walichangia kama ifuatavyo;

Ushauri

Mhe. Mkuu wa Wilaya alishauri kuwa Mji bado ni mchafu hivyo tuendelee kuhamasisha usafi katika maeneo ya Migahawa , mitaro sambamba na ukusanyaji wa fedha ya taka.

KU/SMC/BM/86/2022 – TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI YA OKTOBA- DESEMBA 2021.

A. KAMATI YA UKIMWI

Mwenyekiti wa kamati ya UKIMWI aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya UKIMWI kwa kipindi cha robo ya nne ya April – Juni 2022.

Taarifa ilipokelewa

B: KAMATI YA UCHUMI AFYA NA ELIMU

Mwenyekiti wa kamati ya Uchumi Afya na Elimu aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Uchumi Afya na Elimu kwa kipindi cha robo ya nne ya April – Juni 2022.

Tarifa ilipokelewa

C: KAMATI YA MIPANGO MIJI

Mwenyekiti wa kamati ya Mipango Miji aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Mipango Miji kwa kipindi cha robo ya nne ya April – Juni 2022.

Taarifa ilipokelewa

D: KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI

Mwenyekiti wa kamati ya Fedha na Uongozi aliwasilisha taarifa ya utekelezaji kazi za kamati ya Fedha na Uongozi kwa kipindi cha robo ya nne ya April – Juni 2022, Wajumbe walichangia Kama ifutavyo:

Hoja

Mhe. Mnanka alipenda kufahamu ni lini Waheshimiwa Madiwani watafanya ziara ya mafunzo

Jibu

Mwenyekiti aliwaambia wajumbe kuwa bado wanafuatilia kibali Ofisi ya Mhe. Mkuu wa Mkoa.

Hoja

Mhe. Kimamala alipenda kufahamu vikao vingapi katika robo vimefanyika?

Jibu

Mstahiki Meya aliwaambia wajumbe kuwa katika robo ya nne jumla ya vikao vitatu vimefanyika ni tatizo la uandishi.

Taarifa Ilipokelewa .

KU/SMC/BM/87/2022 TAARIFA YA MIRADI YA MAENDELEO

Afisa Mipango Takwimu na Ufuatailiaji aliwasilisha taarifa ya Utekelezaji kazi Miradi ya Maendeleo kipindi cha robo ya nne ya April - Juni 2022.

Taarifa Ilipokelewa.

KU/SMC/BM/87/2022 TAARIFA MBALIMBALI

A. MAPENDEKEZO YA MATUMIZI YA FEDHA ZA 40% ZITOKANAZO NA MAPATO YA NDANI KWA KILA MWEZI

Mkurugenzi aliwasilisha mapendekezo ya matumizi ya fedha za 40% zitokanazo na mapato ya ndani kwa kila mwezi na wajumbe walichangia kama ifuatavyo;

Hoja

Mhe. Kimamala alipenda kufahamu kuhusu kiwanda cha tofali je kimewekewa bajeti ya Fedha kiasi gani?

Jibu

Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa Kiwanda cha tofali kimetengewa bajeti ya Tsh. Milioni 25 kwa ajili ya miundombinu na uendeshaji.

Hoja
Mhe. Chakupewa alipenda kufahamu kuhusu Miradi iliyotengewa bajeti kwa ajili ya kupitiwa na Mwenge.

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa Fedha hii ni kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Mwenge wa Uhuru.

Pongezi
Mstahiki Meya alipongeza taarifa hii.

Taarifa ilipokelewa.

B. MWONGOZO WA UBORESHAJI WA UTENDAJI KAZI KWA KUPIMWA KWA VIGEZO KWA WATUMISHI WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA KWA KIPINDI CHA 2022/2023

Mkurugenzi aliwasilisha Mwongozo wa Uboreshaji wa utendaji kazi kwa kupimwa kwa vigezo kwa Watumishi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa kipindi cha 2022/2023 na wajumbe walichangia kama ifuatavyo;

Ushauri
Mhe. Kafumu alitoa ushauri kuwa kigezo cha usimamizi wa utekelezaji wa Wananchi katika uchangiaji wa miradi ya maendeleo itakuwa ngumu kutekelezeka kwa sababu katika maeneo yetu kuna maboma mengi ambayo hayajakamilika.

Taarifa ilipokelewa.

C. KUWASILISHA MPANGO WA UTOAJI MIKOPO YA SERIKALI ISIYO NA RIBA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mkurugenzi aliwasilisha mpango wa utoaji mikopo ya Serikali isiyo na riba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Taarifa ilipokelewa.

D. TAARIFA YA TATHIMINI YA SENSA YA VYANZO VYA MAPATO VYA HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA KWA KIPINDI CHA 2022/2022

Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ya tathimini ya sensa ya vyanzo vya mapato vya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga kwa kipindi cha 2022/2022 na wajumbe walichangia kama ifuatavyo;

Hoja
Mhe. Anna Mwamba alipenda kufahamu kuhusu mchakato wa kupata dampo la kisasa eneo la Mbarika.

Jibu
Mkurugenzi aliwaambia wajumbe kuwa kutengeneza dampo la kisasa ni gharama kubwa inakadiliwa kifika bilioni 40 lakini kwa sasa tunatafuta fedha ya kufanya maboresho angalau tuweke uzio kuzunguka eneo la dampo.

Ushauri
Wahemiwa Madiwani walishauri kuwa tufanye kampeni za usafi katika maeneo yetu.

Taarifa ilipokelewa.

E. KUWASILISHA TAARIFA YA MAREJESHO KWA VIKUNDI SUGU NA VIKUNDI VILIVYO NDANI YA MUDA 2021/2022

Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ya marejesho kwa vikundi sugu na vikundi vilivyo ndani ya muda 2021/2022 na wajumbe walichangia kama ifuatavyo;

Ushauri
Mhe. Chekwe alishauri kuwa vikundi vipo kwenye mitaa hivyo visifutwe tuendelee kufuatilia.

Taarifa ilipokelewa.

F. RASIMU YA SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI

Mkurugenzi aliwasilisha taarifa ya rasimu ya sheria ndogo za Halmashauri.

Taarifa ilipokelewa.

SALAMU ZA VIONGOZI MBALIMBALI

A. MHE. MKUU WA WILAYA

Mhe. Mkuu wa Wilaya alipongeza Manispaa kwa kukusanya zaidi ya asilimia mia pia alipongeza mikakati ya uondoshwaji wa taka na mpango wa bajeti wa mwaka 2022/2023. Pia aliwaomba Waheshimiwa Madiwani watoe ushirikiano katika marejesho ya mikopo ya 10% na chanjo ya UVIKO.

B. AFISA SERIKALI ZA MITAA

Afisa Serikali za Mitaa alipongeza Manispaa kuwa na mikakati mizuri ya ukusanyaji wa mapato hasa katika zoezi la sensa ya mapato, aliomba wataalam kufanya kazi kwa ushirikiano ili mpango uweze kutekelezeka.

C. SALAMU ZA CHAMA

Mwenyekiti wa Chama alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na Afya anaotupatia pia aliomba kila mmoja kwenye sekta yake awajibike kutekeleza Ilani ya Chama.

KU/SMC/BM/89/2022 – TAARIFA YA MSATHIKI MEYA
Mstahiki Meya alitoa taarifa kuwa Baraza lilijigeuza kuwa Kamati ambapo katika kikao hicho alitangaza kuwa Wakuu wa Idara wanne wamethibitishwa ambao ni;

i. Mkuu Kitengo cha Ukaguzi wa ndani – ndg. Deogratias Masalu
ii. Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi - ndg. Asha Milasi
iii. Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano – ndg. Khadija Dalasia
iv. Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi – ndg. Eliud Fungo

Pia alitoa taarifa kuhusu kumsimamisha kazi kwa kipindi cha miezi miatatu kupisha uchunguzi Muuguzi wa Zahanati ya Mtimbwa ndg. Maclina Gwido Mduda.

KU/SMC/BM/90/2022 – KUFUNGA KIKAO:
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri ambayo ina nia ya kuiletea maendeleo Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 9.10 Alasiri.

Umesambazwa na ……. Saini ……. Tarehe ……

UMETHIBITISHWA / HAUKUTHIBITISHWA

……...	……..
Jacob J. Mtalitinya	Mhe. Jastin Malisawa
Mkurugenzi Manispaa	**Mstahiki Meya**
KATIBU	**MWENYEKITI**